VITABU VYA KUTAFASIRIWA NA FASIHI YA KISWAHILI

na

Bi. Sheila C.W.A. Ryanga

## Foreward

Recently, in the University of Nairobi a debate has emerged concerning whether or not books translated into Kiswahili are admissible in Kiswahili literature. Bi. Ryanga, in this paper, examines the extent to which such books have contributed to literature in Kiswahili and the sources of the shortcomings associated with them. She argues that literature concerns itself with the values, activities and aspirations of a people. The eloquence and fluency in the language employed is critical toward that goal. Translations have the potential for enhancing the recipient literature but may also affect it adversely.

Ms. Ryanga's paper demonstrates that historically worldwide translations have been integral in all traditions of literature including literature in Kiswahili. Examining the phases in the development of literature in Kiswahili in Kenya it is observed that translated books have mirrored and contributed to the broad themes of colonial, independence and neo-colonial experiences. According to the author many of the shortcomings associated with books translated into Kiswahili originate from inexperience of translators and the unavailability of proper tools of translation, i.e. good dictionaries and other references, and unrefined professional standards of both translators and publishers. However, a few exemplary works are available. The author suggests that the status of translations in Kiswahili could be improved tremendously given the above weak points by: 1) providing professional training for translators; 2) entrusting the task of publication to competent editors and publishers; 3) and strengthening the teaching of translation skills in secondary and university curriculum. Hence, such books of translation into Kiswahili should not be rejected indiscriminately in Kiswahili literature.

* * *

Hivi majuzi miongoni mwa wana-chuo katika idara ya lugha chuo kikuu cha Nairobi, kulizuka mjadala kuhusu kukubaliwa kwa vitabu vilivyotafasiriwa kwenye fasihi ya Kiswahili. Mjadala huo una madai kwamba vitabu vilivyota fasiriwa havina nafasi katika fasihi ya Kiswahili. Dai lingine ni kwamba tafasiri hizo zinaua fasihi ya Kiswahili badala ya kuiendeleza. madai haya yote hutolewa kwa sababu wasomi wa tafasiri hizo za fasihi iliyoandikwa asilia kwa lugha nyingine, huwa hawaoni mnato wala ladha yoyote ya Kisanaa kwenye kazi hizo. Nyingi ya kazi zilizotafasiriwa lugha yake huwa ya kiwango cha chini. Lugha inayotumika huwa haina ufasaha kama lugha kwenye tungo asilia. Kwa ajili hii, maudhui ya tafasiri hayaendelezwi vyema, na maana au ujumbe unaowasilishwa mara nyingi inapotoka.

Jambo jingine katika madai yanayowasilishwa na wana-chuo, linahusu ufunzaji wa uchambuzi wa vitabu vya fasihi vilivyo-tafasiriwa. Dai hasa ni kwamba matumizi ya lugha katika kazi hizi hutatanisha wakufunzi pamoja na wakurufunzi. Kwa mfano, kwenye mataala wa fasihi darasani, mkufunzi anapowaambia wanafunzi wachambue matumizi ya lugha, mtindo, na mbinu za mwandishi hali kitabu kihusikacho kimetafasiriwa, hapo mwanafunzi atakuwa anachambua umbuji wa mtunzi ama mfasiri? Hili ndilo jambo linalokanganya.

<u>Kiini Cha Dosari</u>

Kwamba vitabu vya fasihi vilivyotafasiriwa kwa Kiswahili vina dosari ni jambo lisilokanushika. Mambo muhimu yanayoji-tokeza kama dosari hasa itaonekana ni katika upande wa sarufi, matumizi ya lugha na mantiki - yaani ukosefu wa uthabiti katika uwasilishaji wa ujumbe asilia kwenye tafasiri.

Mpaka sasa uchunguzi haujafanywa juu ya nyanda hii ya tafasiri; uchunguzi ambao ungefichua vile mambo yalivyo hata kusababisha mjadala wa aina hii miongoni mwa wasomi wa fasihi. Utafiti pia haujafanywa kuhusu sababu za kujikita kwa dosari hizo kwenye tafasiri, dosari ambazo zinawaathiri wale wanaokataa kuvikubali vitabu vya tafasiri katika fasihi ya Kiswahili.

Kwanza ni bora kutafuta kiini cha dosari hiso ili kuvumbua dosari zilizojificha, ndivyo zitazamwe kama zinaweza kurekebishika. Pili, dosari hizo zichunguzwe kama kwa hakika zina uzani wa kusababisha tafasiri za vitabu vya fasihi kutupliwa nje ya fasihi ya Kiswahili. Kulingana na hoja zilizotangulizwa, tuna haki ya kujiuliza kama inahalisi kuvitweza vitabu vya tafasiri na kuviondoa kwenye fasihi. Inafaa utafiti ufanywe kufuatia taratibu maalumu hadi maafikiano ya kuzikataa ama kuzikubali tafasiri katika fasihi. Bila hivyo, hoja na madai ya wapinzani hayatakuwa na msingi.

Msingi wa Fasihi

Kabla ya kujadili hoja zilizotangulia kuelezwa, nitazungumzia kwa muhtasari mambo mawili muhimu: - kwanza ni jukumu la fasihi, pili ni jukumu la tafasiri. Fasihi hujishughulisha na taratibu za jumuiya. Fasihi ni kazi ya sanaa iliyochukua jukumu la kutudhihirishia na kututatulia hali zetu za kisiasa, kijamii, na utamaduni kwa jumla. Ni yakini kwamba fasihi ni mdhihirisho ama kiyoo cha maisha ya jamii na uhusiano wao katika muktadha wa mazingira na maumbile yao. Hivyo fasihi inafunza na kutumbuiza. Maelezo haya yanamaanisha kwamba maendeleo ya fasihi hayana budi kuzingatiwa kuambatana na mujibu wa maendeleo ya jumuiya yenyewe na utamaduni wake. Moja kati ya sifa za fasihi ni matumizi mazuri ya lugha. Neno "fasihi" limetokana na ufasaha wa lugha. Ufasaha wa lugha huendeleza umbuji wa mwandishi kwa kutiririsha kadhia zake vizuri. Ikiwa lugha si sahihi, basi sanaa ya fasihi haitapendeza kimantiki, kilugha na hata kisanaa.

Jukumu la tafasiri nalo limeambatana sana na lile la fasihi. Tafasiri ina madhumuni ya kuwawasilishia ujumbe wa manufaa kwa watu ambao hawafahamu lugha asilia iliyotumika kwenye maandishi yanayohusika. Kwa ajili hii, tafasiri pia inatambulikana kama kazi ya kisanaa kama sanaa ya fasihi, kuchora ama kusana sanamu. Sanaa ni kipawa cha mtu binafasi. Kila mtu hanacho hicho kipawa kimoja tu, bali vipawa tofauti; wengine kuchora picha, wengine kujenga na kadhalika. Baadhi ya watu wanaweza kuzimudu sanaa kadha wakati mmoja, lakini si kazi rahisi. Kwa mfano wengine wana kipawa cha utungaji, wengine cha kutafasiri. Basi, ikiwa hatuna kipawa cha aina moja, mradi kuridhika na kile tulichopata. Tunaloweza hapo ni kuathirika na kufurahia wanaotumia vipawa vyao vingine ili kutufunza na kutufurahisha sisi tusiozitaili fani hizo.

Inaposemekana kwamba vitabu vya fasihi vilivyotafasiriwa vikubaliwe katika fasihi ya Kiswahili, inatupasa kuzingatia shuruti zake ambazo lazima zitimizwe kabla ya kutekeleza mujibu huu. Kunayo mambo manne ya kujipimia mfasiri:

1. Ufahamu mkamilifu wa ujumbe asilia na jinsi ya kuueleza katika lugha pokezi.

2. Umahiri na hisi za kisanaa za mfasiri.

3. Ujuzi wa lugha fasaha - lugha pokezi na lugha asilia.

4. Ufundi wa mfasiri katika mbinu na taratibu za sanaa hii, na pia somo analolitafasiri.

Vitabu vya tafasiri pamoja na tungo asilia za fasihi zinatumika na kusomwa na watu wengi sana. Hivyo kila mtekelezi wa sanaa hizi hadi azingatie jambo hili ili ajitokeze na kazi za kisanaa zisizotweza taaluma hizo wala kuaibisha lugha iliyotumika. Tuzingatiapo haya yote, ndipo inapotuhalisi kujipurukusha na kusuluhisha mjadala huu kwa ajili ya kuleta maafikiano baina ya wana-fasihi na wana-tafasiri.

Orodha ya Kanuni

Ili vitabu vya tafasiri vikubaliwe kwenye fasihi mradi tujiulize swali hili: Je, vitabu vilivyotafasiriwa vinakidhi dhima ya fasihi ya Kiswahili? Mapisi ya mtaala wa fasihi ulimwenguni yanadhihirisha kutumiwa kwa vitabu vya tafasiri katika fasihi ya lugha iwayo yote ile, iwe ni fasihi ya Kiingereza, Kirusi, Kifransa na kadhalika. Kwa hivyo matumizi ya tafasiri kwenye fasihi si jambo geni. Ikiwa fasihi ya Kiingereza na Kifransa imeruhusu tafasiri za lugha nyingine zitumike katika somo la fasihi yao, kwa mfano: Odyssey na Iliad, vitabu vilivyoandikwa asilia kwa Kigiriki; The Government Inspector, ambacho kiliandikwa asilia kwa Kiruai, The Plague, The Houseboy, n.k., vilivyotafasiriwa kutoka Kifransa, sioni ni kwa nini hatua hii ikataliwe kwenye fasihi ya Kiswahili. Kukataliwa kwake bila shaka kunasababishwa na mambo mengine yaliyomo katika tafasiri zenyewe wala siyo ile dhana ya tafasiri peke yake.

Vitabu vya fasihi ya lugha ngeni vinapotafasiriwa huendeleza jukumu la fasihi na kupanua maudhui yake katika ile lugha ya tafasiri; maudhui kama ya kiijitimai, ya kufurahisha, ama tasnifu itekelezayo maslaha ya jumuiya nzima. Ikiwa vitabu hivyo havikidhi haja au dhima ya fasihi kama inavyoendelezwa katika lugha pokezi, basi itakuwa sawa kuvizuiya visitumiwe katika somo la fasihi la lugha inayohusika.

Sababu ya lugha nyinginezo kukubali vitabu vya tafasiri ni kwamba tafasiri hizo husaidia kupanua mawazo na fikira za wasomi pamoja na jamii ya waandishi: kimtindo, tasnifu, umbuji na matumizi mbali mbali ya lugha. Kazi za tafasiri hupanua ujuzi wa kisanaa, na kuwaelimisha wasomi juu ya maisha ya watu wanaoishi katika mataifa na tamaduni nyinginezo. Tena tafasiri hazipanui mawazo tu bali huwapa waandishi fikira mpya, uvumbuzi wa mbinu mpya za kisanaa na kuwaathiri kufanya majaribio ya mbinu ngeni katika maandishi yao wakitumia lugha yao asilia. Hii ni faida inayoongeza hazina ya elimu katika kuzijua jumuiya mbali mbali, na kuzilingasnisha na zetu ili kukadiria maendeleo tunayoyatarajia kisiasa, kijamii na kielimu. Hili pia ni jukumu la fasihi.

Matumizi ya vitabu vilivyotafasiriwa kwenye fasihi ya Kiswahili hayaanzi sasa kufikiriwa. Ushirikiano huo ulikuweko tangu zamani. Kwa hivyo pengine mjadala ungeelekea upande wa "kuondolewa kwa vitabu vya tafasiri katika fasihi ya Kiswahili" wala siyo, "kukubaliwa kwa vitabu vya tafasiri katika fasihi ya Kiswahili." Ninasema hivi kwa sababu tunapochunguza maandishi ya fasihi ya Kiswahili, itaonekana kwamba vitabu vya tafasiri vilikuwa vikitumika tangu zamani, ambapo fasihi kwa lugha ya Kiswahili ilikuwa bado katika kiwango cha kufurahisha tu, bila jukumu hasa la kuwaelimisha wasomi juu ya maisha yao katika mazingira wanamoishi.

Baadhi ya tafasiri zilizokuwa zikitumika tangu zamani ni: Hekaya za Abunuwasi, Alfu - lela - Ulela, Elisi katika Nchi ya Ajabu na vitabu vinginevyo. Tafasiri hizi ziliingizwa katika fasihi ya Kiswahili tangu awali. Baada ya muda, baadhi ya waandishi kwa kugha ya Kiswahili waliathiriwa na fasihi hiyo. Athari hizi zadhihirika katika hadithi zilizobuniwa na waandishi chipukizi wa Kiswahili kama mwandishi maarufu Shaaban Robert: Kusadikika, Adili na Nduguze; halafu Kurwa na Doto, ya M.S. Farsy; Nahodha Fikirini, ya Ali Jamadaar; Kisima cha Giningi, ya Mohamed S. Abdalla. Si ajabu basi kuona siku hizi vitabu vya tafasiri vikienea na kuathiri fasihi ya Kiswahili kila upande, - tamthilia, riwaya na hata ushairi (arudhi za ushairi wa Kiswahili zaonyesha athari za kigeni.) Mfano tafasiri kama Mabepari wa Venisi, Juliasi Kaizari, Mfalme Idipode, na Wema Hawajazaliwa, zinazotokana na mataifa mengine barani Afrika na Ulaya, zinatekeleza jukumu la kuijenga fasihi ya lugha inayofanyiwa tafasiri na kuanua daraja yake kisanaa na kitamaduni.

Sababu mojawapo ya kuenea kwa vitabu vya tafasiri kwenye fasihi ya Kiswahili ni upungufu wa vitabu vya tungo asilia ambazo zinatosheleza wadhifa wa fasihi kikamilifu. Nasema haya hasa ninapofikiria kiwango cha maandishi ya fasihi ya Kiswahili nchini Afrika ya Mashariki - kimaudhui, ufasaha wa lugha - kiwango ambacho kitakidhi watu wa daraja mbali mbali za mtaala huo. Ni kweli basi kusema kuwa kuwako kwa vitabu vilivyotafasiriwa kama ziada ya vitabu vya fasihi ni jambo la maslahi, uongofu na maendeleo ya fasihi kwa jumla. Hivi nakubaliana na maoni ya Kazungu na Mazrui:

> Kwa bahati mbaya watu wengi leo wanazikataa tafasiri hizi na kudai kuwa haziingii katika fasihi ya Kiswahili. Lakini endapo tafasiri hizi zimetumia lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa mbinu zake za kifasaha, basi kitendo cha kuzitoa katika fungu la fasihi ya Kiswahili kitakuwa ni cha taasubi tu kisichokuwa na mantiki yo yote.

Aya ya Fasihi

Sasa nitachukua fursa hii kuchambua kwa ufupi maudhui machache yaendelezayo fasihi ya Kiswahili kama ilivyo leo katika nyanja ya riwaya na tamthilia. Ili kutekeleza uchambuzi huu sawia, nitagawanya fasihi katika mafungu matatu:

1. Fasihi wakati wa ukoloni

2. Fasihi baada ya uhuru

3. Fasihi juu ya ukoloni mambolea.

Kabla ya ukoloni, maudhui ya tungo asilia yalielekea upande wa kufurahisha katika riwaya na tamthilia. Kwa mfano, Nakupenda Lakini . . . ni mchezo unaotongoa maisha ya kijamii, lakini maudhui yake si mazito kama ya kujitafiti, uzandiki na mengineyo. Hali kadhalika, ziko tafasiri zilizofanywa kutoka lugha nyingine kama Kiingereza - Elisi katika Nchi ya Ajabu; na kutoka Kiarabu kama, Hekeya za Abunuwasi. Maudhui ya tafasiri hizi ni ya kuwafurahisha wasomi walioandikiwa - kuwapatia watu fursa ya kusoma fasihi isiyohitaji uzito wa fikira kwa kuyaelewa yanayoendelezwa vitabuni humo.

Baadhi ya vitabu vilivyofasiriwa siku hizo, vinaonyesha maudhui yanayowatwaza wazungu, kuonyesha ustaarabu na uwezo wao, huku wakiwatweza Waafrika na kuwonyesha uduni wao. Maudhui haya yanapatikana kwenye tafasiri ya Kisiwa Chenye Hasina; na Mashimo ya Mfalme Suleiman.

Fasihi baada ya uhuru ilifuata mkondo wa kuonyesha ubovu na udhalimu wa wakoloni na ukoloni wao. Waandishi asilia katika lugha ya Kiswahili walijitoa katika lindi la kuonyesha mwamko wa Waafrika katika kuutetea na kuupata ukombozi wao, huku wakionyesha kila aina ya uonevu walioufanyiwa na wakoloni. Mfano ni Ebrahim Hussein katika Kinjeketile; Mugyabuso Mulokozi, katika Mkwawa wa Uhehe. Tafasiri ziendelezazo maudhui haya pia zilichipuka: kwa mfano ni Mchimba Madini, na Boi.

Kundi la tatu lina maandishi asilia na tafasiri pia. Tasnifu za vitabu hivi zaidi ni juu ya ukoloni mamboleo, unyanyasi wake, mifumo ya kisiasa na sera za jamii katika nchi zilizojipatia uhuru. Baadhi ya vitabu vya tungo za fasihi ni Mashetani; Nyota ya Rehema ya Mohamed S.M., na asali chungu ya S.A. Mohamed, n.k. Tafasiri zinazojidhihirisha na maudhui haya ni kama Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Nikolai Gogol. Tamthilia hii ilitafasiriwa kwa Kiswahili kutokana makala ya Kiingereza ambayo pia ilitafasiriwa kutokana na Kirusi kilichokuwa lugha ya tungo asilia. Tafasiri nyingine ni kama: Mabepari wa Venisi na Juliasi Kaizari za William Shakespeare, zilizotafasiriwa na J. Nyerere; Wema Hawajazaliwa cha Ayi Kwei

Armah, kilichotafasiriwa kutokana na tafasiri ya Kiingereza ambapo makala asilia yalikuwa katika lugha ya Kifransa.

Tasnifu za vitabu hivi vya tafasiri zinaeleza tabia mbali mbali za kijamii zinazoendelea katika mataifa na tamaduni nyinginezo. Hii hutupa nafasi ya kujichunguza na kupanua mawazo ya jamii zetu katika mazingara yetu. Licha ya hivyo, hata tunapochambua uketo wa tafasiri hizo, zitatuonyesha uzandiki, ufisadi, ubwanyenye - yaani uonevu uliojikita katika jamii ya kila nchi - hali ambayo inapatikana miongoni mwa nakii nyingi za nchi huru za Afrika. Uketo huo pia unajitokaza katika tungo za Kiswahili zisizokuwa tafasiri. Wasomi wa fasihi asilia pamoja na tafasiri wanapata kuelimishwa na kuweza kuona hali ya jumuiya ya kisiasa na kijamii katika muktadha wa Bara zima la Afrika, na hata kwingineko, ulimwenguni. Jambo hili linatudhihirishia kwamba tabia za maisha ya jamii mbali mbali zimejikita katika nafsi za binadamu wote bila kuzingatia nchi zilizowalea; iwe ni Uzunguni, Uarabuni, Merikani ama Afrika.

Fasihi ya Siasa

Vitabu vingi vya fasihi, tafasiri na tungo asilia vinaonyesha jinsi watu wanavyokata tamaa au, jinsi wanavyoona uongozi wa nchi zao aidha ukijikita kwenye mataribushi ya wakoloni ama kuzusha dhuluma zao mpya za kuwanyanyasa wazalando wenzao. Ubinafsi hapa unajitokeza. Ayi Kwei Armah katika kitabu chake Wema Hawajazaliwa, anaonyesha kukata tamaa kwa raia juu ya uongozi wa serikali yao mpya baada ya mapinduzi. Ebrahim Hussein, kwenye Mashetani anaonyesha mabwana wapya jinsi wanavyochukua mahali pa wakoloni - kwa sababu ya athari za kigeni. Mohamed, S.M. katika Nyota ya Rehema anaonyesha vile Waafrika wenye vyeo wanavyowadhulumu wengine wasiopata kubahatika maishani mwao. Ndiposa nikasema vitabu vilivyotafasiriwa vina jukumu la kuiendeleza fasihi ya lugha ambayo inafanyiwa tafasiri. Mradi wanachuo wa fasihi ya Kiswahili kukagua ni vitabu vipi vya tafasiri vinavyokidhi matarajio ya wasomi fasihi ya lugha inayohusika.

Katika kujadili kwangu mjadala huu, sitaki nifahamike vibaya kwamba natetea kazi za tafasiri kiasi cha kutozitoa makosa. La. Kwamba tafasiri nyingi za Kiswahili zina dosari ni kweli. Dosari zenyewe zinajitokeza katika sehemu za uthabiti - kuhifadhiwa kikamilifu kwa ujumbe asilia kwenye tafasiri; na upande wa ufasaha wa lugha.

Malalamiko mengi kuhusu undani wa vitabu vya tafasiri ni kwamba, kwanza inasemekana kuwa havina lugha fasaha yenye ladha, mtiririko wala msamiati ufaao. Pili, kwamba tafasiri hazina uthabiti katika ujumbe uwasilishwao, aidha zinaacha

dhana nyingine nje ya tafasiri au kuwa na ziada ya maoni ya kibinafsi na hisi ambazo hazikudhamiriwa na mwandishi asilia.

Ni kweli kwamba kazi nyingi za tafasiri zina dosari hizo mbili. Mara nyingi mambo hayo hutukia bila ufahamu wa mfasiri mwenyewe. Lakini, wakati mwingine haya hutokana na juhudi za mfasiri kujaribu kufafanua ujumbe wa mtunzi. Kadri anavyofanya ufafanuzi huo, huweza kuacha vifungu anavyoviona vigumu kuvieleza kwa usahihi katika lugha anayoifanyia tafasiri. Jambo la kusema hapa ni kuwa ingewapasa watu wenye maoni haya kwanza wazingatie masharti na matatizo yanayoambatana na kazi ya kutafasiri. Kwa sababu tafasiri ni kazi ambayo inafanyiwa maandhishi ambayo yamekwisha kutungwa na msanii mwingine, kinyume cha tungo asilia, basi si ajabu kusema kwamba daima kutakuwa na tofauti baina ya aina hizo mbili za maandishi. Isipokuwa tofauti hii si lazima iegemee kwenye upande wa tafasiri mbaya. Kama vile ambavyo tungo asilia zisifiwazo kwenye fasihi hutegemea uzuri na ufasaha wa matumizi ya lugha, pamoja na mbinu za kisanaa, (siyo maelezo ya kadhia tu) vile vile tafasiri hutegemea hayo. Kama vile ambavyo mtunzi akikosa kuimudu lugha kwa ufasaha, akiwa hawezi kuendeleza sawia sanaa yake wasomi wake huyaona maandishi yake yakichosha, hali kadhalia mfasiri, kazi yake na wasomi wake. Wasifu wa tafasiri kama kazi nyingine za kisanaa unatokana na utamu na mdundo wa lugha ilitoyumiwa, mfululizo wa taswira na jazanda zikubalikazo katika lugha pokezi, mtiririko wa kadhia na uhifadhi wa ujumbe. Inapasa kufahamika kuwa uthabiti kwenye tafasiri ndio unaowapendeza wasomi.

## Msiba wa Mfasiri

Sasa natutazame mfasiri na matatizo yanayomsibu kazini mwake. Tatizo la kwanza ni lile jukumu la kusoma maandishi asilia ya lugha nyingine hadi ayafahamu kinaganaga yanavyoendelezwa, halafu aweza kuyafikiria katika lugha ya tafasiri. Yapasa kufahamu pia muktadha wa maandishi hayo asilia ili usaidike kuielewa lugha ya mwandishi - ufahamu kama mwandishi ametumia lugha nzito yenye hisia, au lugha nyepesi isiyohitaji fikira za msomaji. Pili, ni kwamba mara nyingi lugha asilia pamoja na ile ya tafasiri huwa zote ni lugha za kujifunza za mfasiri - hapana moja ambayo ni lugha yake ya malezi - hivyo ujuzi mzuri wa lugha zote mbili lazima uweko ama sivyo, vikwazo vitatokea katika ufanyaji kazi hiyo. Haya ni kinyume cha mtunzi asilia. Huyu huwa yale maudhui anayoyaandika ni yake binafsi, yeye ndiye aliyeyaibua; aliyounda kwa dhamira yake wala hana haja ya kuyaambatanisha na mawazo ya mtu mwingine. Pia ujuzi wa lugha unaohitajika ni ule wa lugha moja aliyochagua kuitumia kwa kuandika kadhia zake. Aghalabu, vitabu vilivyotungwa asilia pia huwa na dosari kwa kiasi fulani. Sasa ikiwa mtungaji asilia huweza kuona ugumu na kughafilika katika matumizi ya lugha fasaha, ni

mara ngapi kwa mfasiri anayehitajika kufikiria katika lugh mbili wakati anapofanya kazi yake?

Tatizo lingine kwa mfasiri linahusu msamiati amba utaweza kuwasilisha maudhui ya mwandishi katika uzito a wepesi wake; msamiati ambao utawaridhisha wasomi wa tafasir kama vile maandishi asilia yanavyowaridhisha wasomi wake Utatuzi wa tatizo hili unategemea waledi wa mfasiri katik mbinu za utekelezaji wa tafasiri. Ugumu hutokea ambapo misem au maneno mengine hayelezeki kirahisi katika lugha ya tafasir aidha kwa sababu dhana za misemo hiyo hazipatikani katik lugha pokezi, ama pengine tafsiri zilinganazo na dhana hizo z lugha asilia hazipendezi zikitumika katika lugha nyingine.

Mfasiri mwaledi lazima awe na lugha yenye mdundo inayoeleweka kinaganaga, aweze kujenga kadhia za tungo asili vizuri bila hali ya pindipindi. Haya yote yatekelezwap tafasiri itaonekana nzuri ya kuwapendeza wasomi. Ndiyo pos tafasiri zinazofanywa kwa Kiingereza kutoka lugha nyinginez kama vile; <u>The Plague</u> ya Camus; <u>Crime and Punishment</u> ya Leo Dovesku, zilitungwa asilia kwa Kifransa na Kirusi zinazosomek na kupendeza kama tungo asilia. Ni nadra wasomi wavy kutambua ni tafasiri. Sasa swali la kujiuliza sisi ni hili Kwa nini tafasiri za Kiswahili haziwi hivyo?

<u>Masharti ya Mfasiri</u>

Hapa naifahamike kuwa wale wanaofanya tafasiri z Kiingereza, huwa watu waliofuzu katika mbinu za taaluma hii y tafasiri. Wao huwa weledi wa kazi yao. Ni kawaida kuwa kil mfasiri huichukua sanaa hii kama kazi yake maalumu, n hutafasiri makala ya somo analolifahamu sawasawa. Wafasiri w vitabu vya fasihi kama wengineo huwa ni wana-fasihi na wanaju matarajio ya wasomi wa mtaala huo. Pia wafasiri hao hupat msaada wa makamusi na orodha za maneno za somo walifanyial kazi, maneno ambayo yameelezwa maana sake mbali mbali, kuto maneno yote yaliyokaribiana kimaana (synonyms), na pia kuto mifano jinsi maneno hayo yanavyotumiwa katika sentensi am muktadha upasao: mfano ni kamusi la <u>The Pan Dictionary o Synonyms and Antonyms</u>, lililohaririwa na Laurence Urdangan Martin Manser (1978); <u>The Concise Oxford Dictionary of curren English</u> lililohaririwa na Fowlar, N.W. na Fowler, F.G. Zaid ya hayo, wanayo makamusi yanayoelezea maana kwa lugha mbili mfano kamusi la Kiingereza a Kispania na kimyume chake.

Wafasiri wa Kiingereza wengi wao huwa wameajiriwa katik kazi hii kwa njia ya kuhojiwa ili kuhakikisha kwamba wanapit masharti yote ya mfasiri. Waajiriwa kama hawa ilihal watakuwa na ujuzi mzuri wa lugha zote mbili bila tashwishi y yote. Kwa ajili hii tafasiri za Kiingereza inaonyesh hufanywa kwa utaratibu fulani, na matokeo hadi yawe mazuri

Wafasiri kwa lugha ya Kiswahili hali yao na jinsi wanavyofanya kazi ni tofauti kwa ajili ya uchanga wa taaluma hii nchini Afrika Mashariki. Ni dhahiri kwamba vitabu vya Kiswahili vilivyotafasiriwa na wageni -- aidha Wazungu ama Waarabu, mfano: Mashimo ya Mfalme Suleiman na Alfu lela Ulela vinasomeka vyema, lugha ya mtiriko kuliko vitabu vinavyotafasiriwa nasi waongezi wa Kiswahili humu Afrika Mashariki, iwe wafasiri hao wanatumia Kiswahili kama lugha yao ya malezi - Abdilatif Abdalla na tafasiri yake Wema Hawajazaliwa au ni wafasiri waliojifunza Kiswahili baadaye - Christon Mwakasaka na tafasiri yake Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Sababu mojawapo muhimu ni kuwa uwanda huu wa tafasiri haujatiliwa maanani hapa. Tatizo letu moja ni hili kwamba mtu ye yote azungumzaye Kiswahili na Kiingereza hujiona tayari anaweza kutafasiri makala yanayohusu lugha hizo. Hivyo, watu vivi hivi (wasio wledi wa sanaa hii); watu wasiofahamu hasa kiini cha sanaa ya tafasiri, wala kuzisoma kanuni na taratibu zake hujibagaza jukumu hilo na matokeo yake ni kuvitweza vitabu vya tafasiri kiasi cha kutatanisha ukubalifu wake katika fasihi ya Kiswahili. Haya huja kwa sababu wafasiri wasiozijua kikamilifu mbinu za taaluma hii, hutafasiri kibubu bila kuzingatia sharti la lahani nyororo na lugha aali katika lugha pokezi.

Inayamkinika, wasomi wengi wa fasihi ya Kiswahili hawakatai fasihi iliyotafasiriwa bali wanalopinga ni hali mbaya ya tafasiri zenyewe. Malalamiko yao ni halali kwani hadi leo, kuna tafasiri chache tu miongoni mwao zikiwa za Mwalimu Julius Nyerere, "Juliasi Kaizari", na Samuel Mushi - Mfalme Edipode", ambazo ukizisoma zinaridhisha, kwamba zimetekeleza mbinu ali ali za tafasiri na kuendeleza maudhui asilia kwa lugha fasaha ya Kiswahili.

Wafasiri kwa Kiswahili ningesema hawajapata uongozi ufaao katika mambo ya tafasiri. Licha ya kutojua undani wa taaluma, hata vifaa vya kuwasaidia pia ni haba. Yako makamusi machache sana ya Kiswahili ambayo yana msamiati utoshelezao. Isipokuwa kwa kamusi ya Kiswahili Sanifu (Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili) hakuna kamusi jingine la Kiswahili peke yake.

Yapo makamusi ya lugha mbili. Kiswahili/Kiingereza na Kiingereza/Kiswahili yaliyosimamiwa na Frederick Johnson. Ukweli ni kwamba makamusi haya yalitolewa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1939. Baadaye yalifanyiwa marudio, na marudio ya mwisho yalifanywa mwaka wa 1973, Sote hapa tutakubaliana kwamba Kiswahili Kilichotumika mwaka huo wa 1973 kilikuwa punguani kuhusu mambo kadha ya ufundi na taaluma mpya mpya. Nisemalo hapa ni kwamba, tangu hapo hadi sasa Kiswahili kimekua mapana na marefu. Lugha ya Kiswahili imepata mapanuzi ya ghafla humu Kenya tangu 1974 ambapo Kiswhili kilipitishwa kuwa lugha ya taifa na lugha ya mijadala bungeni. Tanzania pia Kiswahili kilitwazwa ili kikuzwe na kutumiwa shule kama

lugha ya kufundishia, licha ya kuwa cha matumizi ya jumuiya. Sasa, mageuko haya yote kweli yatatoshelezwa na makamusi ya Johnson F.? Kuna jambo muhimu ambalo lazima niliseme hapa - nalo linahusu uhariri na uhakiki wa vitabu vilivyotafasiriwa kwa Kiswahili kabla ya uchapishaji. Wengi kati ya wachapishaji wa vitabu vya tafasiri hawaonekani kusisitiza uhakiki na uhariri wazo tafasiri bali huendelea kuzichapisha baada ya kuzipitia juu juu kama vitabu vya tungo asilia. Lau kama Wahariri huyashunghulikia makala ya tafsiri, basi pengine wangeliyafananisha na makala asilia kama inavyompasa mhariri wa tafasiri kufanya. Haihalisi kuhariri tafasiri bila kutazama makala asilia. Mhariri anapohariri tafasiri, hasa vitabu vya fasihi anatakikana kuchunguza mtindo wa mfasiri, matumizi aali ya lugha, kulifadhiwa kwa kiini cha hadithi na muendelezo wake sahihi; pia kutazama ikiwa tafasiri inatoa mafunzo yanayoendeleza nyanja ya fasihi kwa wasomi wa lugha upokezi. Upungufu wa kazi ya wahariri huleta dosari mintaarafu kwa sababu mtindo wakuhariri kijuu juu haudhihirishi makosa wala kuhakikisha kwamba maana asilia yamelifadhiwa. Kazi za uhariri namna hii ndizo ziletazo uchapishaji wa vitabu vinavyotatanisha ujumbe na mtiririko wa lugha kwa jumla. Jambo hili huvisha ila sanaa yote ya tafasiri. Ndiposa tunapata wasomi wa "uzuri wa lugha" (Aesthetics) wa K19 na K20 wakisema kuwa kazi za fasihi haziwezi kutafasiriwa. Hawa wanadai kuwa sanaa ya usemi inahusu uchaguzi maalumu na mpango fulani wa msamiati katika sentensi.

## Muhtasari

Kutokana na yote tuliyoyajadili, msimamo wa sawa sawa sasa ni kukubali kwamba vitabu vya tafasiri za Kiswahili havina budi kuwa na dosari kwa sababu, tafasiri si kazi asilia na pengine mfasiri hana tajriba ya somo analolitafasiri, tukiacha kando weledi na hisi za kisanaa. Lakini, yote yanapozingatiwa, hoja hizi haziwezi kufanya vitabu vya tafasiri vikataliwe kwenye fasihi ya Kiswahili. Inayopasa ni sisi wasomi na wahariri, na wenye kutafasiri tuchunguze na kutafuta njia za kurekebisha dosari zijitokezazo humo. Hili jambo la kurekebisha linawezekana.

Utimilifu wa baadhi ya vitabu vya tafasiri na uthabiti wake unapinga maoni ya wasomi fulani wanaodai kwamba Kiswahili hakijitoshelezi kimsamiati - kwa minajili ya kuendeleza fikira ngeni. Ziko tafasiri nzuri za lugha ngeni hadi Kiswahili. Hoja hii inathibitisha vile msamiati wa Kiswahili unavyojengeka, na kuongezeka ambapo bila ongezeko hilo ingekuwa vigumu kueleza habari na fani mbali mbali za lugha nyingine kwa uthabili, ukamilifu na ufasaha wa lugha ya Kiswahili. Ninapofikia mwisho wa mada yangu, ningesema kuwa hakuna ithibati yo yote kuwa kazi za tafasiri haziwezi

kuingizwa kisahihi katika fasihi ya Kiswahili. Na ikiwa wapo watu ambao bado wangependa kuendelea kuvitweza vitabu vya tafasiri, basi kwanza wangejaribu kuangatia matatizo yanayowakabili wafasiri. Ni baada ya kuzingatia hayo ambapo tutafahamu sababu zilizomfanya mfasiri mwalimu Julius Nerere katika kazi yake Juliasi Kaizari (utangulizi wa toleo la pili uk. vi.) kusema:

> Nimetumai nafasi ya mabadiliko haya pia kusahihisha makosa fulani yaliyokuwamo katika toleo la kwanza. Makosa haya yalikuwa ya aina mbali mbali. Pengine nilikuwa nimekosea tafasiri yenyewe; pengine misitari fulani ilikuwa imeachwa; na pengine kulikuwa na makosa ya kupiga chapa.....

Hivyo madai ya kukataa vitabu vilivyotafasirwa kwenye fasihi ya Kiswahili yaongesha dhahiri kwamba wenye nayo wana haja na madhumuni ya kuitekuwa kwa tindo na mitaimbo taaluma na sanaa ya tafasiri.

Mapendekezo:

1. Kuwe na mafunzo maalumu ya wanaotaka kujiungana kazi za kutafasiri ili waweze kufunzwa taratibu na kanuni za tafasiri kwa jumla - ili kila mtu awaye yote asijione yu tayari kutafasiri bila kujipatia ujuzi huko. Masomo haya pia, yamruhusu mfasiri kujifunza mbinu za somo atakalolifanya kazi iwe ni fasihi, makala ya sayansi, sheria n.k.

2. Kuwe na wahariri - wahakiki maalumu wa kazi za tafasiri za masomo wanayoyamudu peke yake. Hivi vitazuiya uchapishaji wa tafasiri zenye kiwango cha chini kwa ukamilifu wake.

3. Mtaala wa tafasiri unahitaji kutiliwa msisitizo katika mafunzo ya lugha kwenye ratiba za shule za upili na hata chuo kikuu. Hatua hii itawafanya watu watilie maanani somo hilo na hivyo kuifikiria taaluma ya tafasiri kama inayohitaji ujuzi maalumu kama kazi za kisanaa nyinginezo.

## MAELEZO

Lugha Pokezi -- Receptor/target language
Lugha asilia -- Source language

## MAREJEO YA VITABU JUU YA TAFASIRI


Achilles, F. "Some reflections on the difficulty of Translation." In Brower, R.A. On Translation. Oxford University Press, New York: 1966.

Ali, C.W. "The Problems of Translating From English into Swahili: As Exemplified by V.O.K. News Items. (M.A. Dissertation -- Unpublished, University of Nairobi, 1981).

________. "Nadharia ya Tafasiri na mbinu zake." (Unpublished manuscript with H.E.B. Publishers.)

Chatman, S. (ed). Literary Style -- A symposium. Oxford University Press, London: 1971.

Harris, L. "Translating Classical Literature into Swahili." In Allen, J.W.T. (ed). Swahili Journal, vol. 37-46 1967-76.

Hyder, M. "Swahili in a Technical Age." In Africa Contemporary Monographs, No. 4. East African Publishing House: 1966.

Nida, E.A. Towards a Science of Translating. Printed in Netherlands, 1964.

Ullmann, S. Words and Their Use. Muller, London: 1951. (Man and Society Series).

Yaa, J.D. A Guide to English/Kiswahili Translation. Comb Books, Nairobi: 1975.


## MAREJEO YA TAFASIRI NA TUNGO ZA FASIHI


Ayi Kwei Armah, Wema Hawajazaliwa, Kimetafasiriwa na Abdilati Abdalla.

Ferdinand Oyono, Boi. Kimetafasiriwa na Raphael Kahaso na Nathan Mbwele.

William Shakespeare, Juliasi Kaizari. Kimetafasiriwa na Julius K. Nyerere.

__________, Mabapari wa Venisi. Kimetafasiriwa na Julius K. Nyerere.

__________, Makbeth. Kimetafasiriwa na Samuel S. Mushi.

Nikolai Gogal, Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kimetafasiriwa na Christian Mwakasaka.

Homer, Odyssey (Utenzi).

__________, Iliad (Utenzi).

Lavis Carrol, Elisi katika Nchi ya Ajabu.

(Unknown), Hekaya za Abunuwasi. Kilitafasiriwa na - The International Language Committee, E. Africa.

Robert Louis Stevenson, Kisiwa Chenye Hazina.

(Unknown), Alfu - hela - Ulela. Kilitafasiriwa na Sir Richard Burton kutoka kiarabu hadi kiingereza.

Sir Rider Haggard, Mashimo ya Mfalme Suleman.

Henry Kuria, Nakupenda Lakini....

Said A. Mohamed, Asali Chungu.

Ebrahim Hussein, Kinjeketile. Oxford University Press.

__________, Mashetani. Oxford University Press.

Peter Abraham, Mchimba Madini.

## MAKAMUSI

A standard English - Swahili Dictionary by the late Frederick Johnson.

A standard Swahili - English Dictionary by the late Frederick Johnson, 1973 (later edition).

The Pan Dictionary of Synonyms and Antonyms. (Eds.) Laurence Urdang and Martin Manser.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu - Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili Dar.

## SHARED PAINS

by

Bogaletch Gebre

This is this land
Where children look like
    shrunken bags
    like old men with no bellies
    their souls hanging
    on a string of skeleton
    with no life force

Where is this land
    my country
    the foot print of time
    museum land
    the story of the earth
    cradle of mankind

How can the nightmare of famine
The agony of starvation
The death of the nation and its future
    unfold under supervision
    of U.N. and relief agencies

I run here and there
    to tell the story of my people
    their plight and desperation
    I prayed and pleaded
    for food and medicine

Where was World Vision
    CARE and AFRICARE
    BARAC and Oxfam
    FAO and UNICEF
    newsreporters and cameramen
    politicians and clergymen
    gobbling up all the donations
    giving out little
    here
    there
    to keep everyone on the borderline
    of starvation

Let me ask
My friends ... observers
    people of this world
    had this pestilence hit Europe and America
    the English or French
    what could have been the response